



Tanzania Forest
Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi
Misitu ya Asili Tanzania



Kampeni ya misitu ya hifadhi kwa kila kijiji

Himiza
Kuanzisha,
Kusimamia
kuendana na misingi
ya Utawala Bora na
Kueneza Usimamizi
Shirikishi wa Misitu
kwa Jamii
(USMJ)

Tamko
namba 6 la Sera ya
Misitu ya mwaka 1998
limeelekeza; - "Misitu ya
Vijiji itasimamiwa na serikali
za vijiji au mamlaka nyingine
zitakazowekwa na serikali za
vijiji zenyewe. Misitu ya vijiji
itasimamiwa kwa ajili ya uhifadhi
au matumizi endelevu kwa
kuzingatia Mpango ya
Usimamizi wa Msitu
husika"

"Kila kijiji chenye
msitu wa asili katika
ardhi yake kina haki
ya kuanzisha, kumiliki
na kusimamia Msitu wa
Hifadhi wa Kijiji kwa
manufaa ya sasa na ya
kizazi kijicho"

Juni, 2020

Kampeni ya Misitu ya Hifadhi kwa kila kijiji

Kuhimiza Uhifadhi na Matumizi Endelevu ya Hekta Million 22 za misitu ambayo ipo kwenye Ardhi ya Vijiji, sawa na asilimia 46 ya Misitu yote Tanzania.

Kwa kuzingatia Maelekezo ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999; Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002, vifungu namba 32 hadi 41– imeweka utaratibu wa kisheria wa kuanzisha Msitu wa Hifadhi wa Kijiji, Msitu wa Hifadhi wa Jamii au Kikundi na Msitu wa Hifadhi wa Mtu binafisi, katika Ardhi ya Vijiji.

MISITU YA HIFADHI ZA VIJJI HUSAIDIA KATIKA HIFADHI YA MIFUMO YA KIIKOLOJIA, NA WAKATI HUO HUO HUCHANGIA MAENDELEO YA JAMII



AFYA



KILIMO



MAJI



ELIMU


UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MISITU



KIJI CHAKO KINA MSITU WA HIFADHI WA KIJIJI?

Bila Kutekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii (USMJ):-

- ❖ Zaidi ya hekta 460,000 za misitu zitaendelea kupotea kila mwaka Tanzania
- ❖ Mapato ya Serikali yatafungua kadiri Misitu inavyozidi kutoweka
- ❖ Uvunaji haramu na usioendelevu utaendelea kufanyika katika misitu iliyo kwenye ardhi ya kijiji ambayo bado haijahifadhiwa kisheria
- ❖ Mapato ya serikali yataendelea kupotea kutokana na uvunaji haramu na ugumu wa kudhibiti biashara ya mazao ya misitu katika maeneo ambayo hayana mpango wa usimamizi wa misitu.




Kwa Kutekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jami (USMJ)

- ❖ Kutaoka zaidi ya hekta milioni 17.6 za misitu sawa na takribani 80% ya Misitu yote iliyo katika ardhi ya vijiji ambayo itarasimishwa kuwa Misitu ya Hifadhi za Vijiji.
- ❖ Kuanzisha Misitu ya Hifadhi za Vijiji kunaleta mapato endelevu kwa Serikali za Vijiji, Serikali za Mitaa na Serikali kuu, kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa misitu nchini na maendeleo ya jamii vijijini na mijini.

ZIJUE MAMLAKA ZA USIMAMIZI WA MISITU NA UKUSANYAJI WA MAPATO YANAYOTOKANA NA MISITU MBALIMBALI TANZANIA

❖ Serikali za vijiji hazina mamlaka ya kukusanya mapato kutoka kwenye Misitu ambayo haijatengwa kuwa Misitu ya Hifadhi za Vijiji, hata kama misitu hiyo ipo katika ardhi ya Kijiji.

❖ Kijiji kinapoanzisha Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kinakuwa na mamlaka ya kukusanya mapato yanayotokana na uvunaji endelevu, uuzaji wa hewa ukaa faini, utalii, na uuzaji wa mazao yasiyo ya mbao, kwa 100%.



❖ Serikali za vijiji zina fursa ya kuhifadhi zaidi ya hekta milioni 17.6 za misitu iliyo katika Ardhi ya Vijiji ambayo bado haijahifadhiwa kisheria kama ilivyoelekezwa katika Tamko namba 5 na 6 la Sera ya Misitu ya mwaka 1998, na kifungu namba 32 hadi 41 vya Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002.

ZIJUE HATUA MUHIMU KATIKA KUENZISHA NA KUSIMAMIA MSITU WA HIFADHI WA KIJJI

Hatua ya Kwanza:

Serikali ya Kijiji kutambua mipaka ya Ardhi ya Kijiji iliyowekwa kwa mujibu wa kifungu namba 7 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999. Halmashauri ya Kijiji kutoa pendekezo kwa mkutano mkuu wa Kijiji, la kuanzisha Msitu wa Hifadhi wa Kijiji, na mkutano mkuu kuridhia pendekezo hilo.

Hatua ya Pili:

Kuchagua Kamati ya Maliasili ya Kijiji kwa kuzingatia malekezo ya kifungu namba 33 (1), (2) cha Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002

- ❖ Wajumbe wa Kamati, wasiopungua 12 wachaguliwe na mkutano mkuu wa Kijiji,
- ❖ angalau theluthi moja wawe wanawake, Kuwe na uwakilishi mzuri kwa kila kitongoji
- ❖ wawe wenye weledi, na waadilifu ikiwezekana wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu vizuri
- ❖ wenye moyo wa kujitolea, waoujua msitu wa Kijiji kwa ufasaha
- ❖ Kamati ichague viongozi (Mwenyekiti, Katibu na Mwekahazina), waadilifu hasa katika maswala ya fedha
- ❖ Uchaguzi wa Mwenyekiti hufanyika kila baada ya mwaka mmoja

Hatua ya tatu:

Kutambua na kuweka alama za Mpaka wa eneo la Msitu wa Hifadhi wa Kijiji. Alama zinaweza kuwa kupaka rangi miti, kuchonga barabara, kuweka mabango na mawe ya mpaka kuzunguka msitu wa hifadhi wa Kijiji. Hii ni pamoja na kuchora ramani ya Msitu wa Kijiji.

Hatua ya nne:

Kuandaa mpango wa Usimamizi wa Msitu wa Kijiji ukijumuisha maelezo ya rasilimali zilizopo, majukumu ya wadau mbalimbali, jinsi msitu utakavyosimamiwa na jinsi uvunaji au matumizi endelevu ya mazao ya msitu yatakavyofanyika. Hatua hii hujumuisha kufanya tathmini Shirikishi ya Mazao ya msitu.

Hatua ya tano:

Kuandaa Sheria Ndogo za Usimamizi wa Msitu kwa kuzingatia maelekezo ya kifungu namba 163 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) 1982, na kifungu namba 34 cha Sheria ya Misitu namba 14, 2002.

Hatua ya Sita:

Kuidhinisha na Kurasmisha. Sheria Ndogo na Mpango wa Usimamizi wa Msitu wa Kijiji huidhinishwa na Kikao cha Halmashauri ya Kijiji, Mkutano Mkuu wa Kijiji na Halmashauri ya Wilaya husika.

Hatua ya Saba:

Utekelezaji - Serikali ya Kijiji kupitia Kamati ya Maliasili inatekeleza Shughuli za Usimamizi wa Msitu wa Kijiji kama vile doria, uvunaji endelevu, kudhibiti moto kichaa, kwa kuzingatia Mpango wa Usimamizi wa Msitu na Sheria Ndogo.

Hatua ya nane:

Kupitia na Kurekebisha - Baada ya angalau miaka mitatu ya utekelezaji, Serikali ya Kijiji kwa Kushirikiana na Wataalamu wanafanya mapitio na kufanya Maboresho ya Mpango na Sheria Ndogo za Usimamizi wa Msitu. Serikali ya Kijiji inapeleka maombi rasmi Idara ya Misitu na Nyuki, kupitia Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, kuomba Msitu wa Hifadhi wa Kijiji Utangazwe kwenye Gazeti la Serikali.

Hatua ya tisa:

Kuendeleza na Kueneza kwenye maeneo mengine.

- ❖ Serikali ya Kijiji kuendelea kusimamia msitu wa Kijiji kwa Kuzingatia Sheria Ndogo na Mpango wa Usimamizi wa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji, na kwa kuzingatia Misingi ya Utawala Bora
- ❖ Serikali ya Kijiji kuongeza Msitu wa Hifadhi wa Kijiji endapo bado katika ardhi ya Kijiji kuna misitu ambayo haijahifadhiwa kisheria
- ❖ Serikali ya Kijiji kuhimiza vijiji jirani vyenye misitu ambayo haijahifadhiwa kisheria kuanzisha Misitu ya Hifadhi ya vijiji vyao

YAJUE MASWALA YA MSINGI KATIKA KUTEKELEZA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA JAMII (USMJ)

1. **USMJ ni utaratibu wa Kisheria** - uliowekwa kupitia Tamko namba 5 na 6 la Sera ya Misitu ya mwaka 1998 pamoja na vifungu namba 32 hadi 41 vya Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2014.
2. **Kupitia USMJ, Serikali za Vijiji zinarasimisha misitu** iliyo katika ardhi ya vijiji, kwa kuanzisha Misitu ya Hifadhi za Vijiji, Misitu ya hifadhi ya jamii (vikundi) au misitu ya hifadhi ya watu binafsi.
3. **Jamii inakuwa mmiliki na meneja wa Msitu:** Kupitia USMJ, Misitu inahifadhiwa ndani ya mipaka ya ardhi ya vijiji tu. Meneja wa Msitu anakuwa kamati ya Maliasili ambayo inachaguliwa na mkutano mkuu wa Kijiji, na husimamiwa na Halmashauri ya Kijiji.
4. **USMJ unatekelezeka kwa misitu ya aina zote;** midogo, mikubwa, iliyo katika hali nzuri, iliyoharibika, ya miombo, mikoko na ya ukanda wa pwani, muhimu tu ni kwamba iwe ndani ya mipaka ya ardhi ya Kijiji.
5. **Malengo ya USMJ** yanaweza kuwa kuhifadhi mifumo ya **kiikolojia**, vyanzo vya maji, kulinda miti ya madawa, kuzuia mmomonyoko wa udongo kuanzisha uvunaji endelevu wa mazao ya mbao au yasiyo timbao, uvunaji wa kibiashara au usio wa kibiashara, au kwa ajili ya ibada, mila na desturi za jadi.
6. **USMJ unaamini katika Mahusiano ya jamii na Msitu**, kwamba misitu hii inapatikana kwenye ardhi ya Kijiji na kwamba wanavijiji wameishi na misitu hiyo tangu zamani– hivyo wana haki ya kuimiliki na kuisimamia kisheria.
7. **Kupitia USMJ, jamii ni wafanya maamuzi na sio walenzi tu.** Msitu wa Kijiji unakuwa mali ya jamii nzima na kusimamiwa kupitia serikali ya Kijiji. Jamii inakuwa meneja, mwenye mamlaka ya kusimamia, kutumia, kuendeleza na kuzuia matumizi yasiyoendelevu au yasiyo na maslahi kwa kijiji.
8. **USMJ unatumia mifumo ya kiserikali iliyopo, hauanzishi mfumo mpya.** Halmashauri ya Kijiji iliyochaguliwa na wananchi wenyewe ndio chombo kikuu cha Usimamizi wa Msitu wa Kijiji, ambapo madaraka haya yanaweza kukasimiwa kwenye Kamati ya Maliasili, ambayo pia uchaguliwa na wananchi. Kijiji huandaa Sheria Ndogo ambazo hurasimishwa na Serikali kuwa na uhalali sawa na Sheria zinazotungwa na Bunge.
9. **USMJ umefanya mamlaka ya Maafisa Misitu kuwa ya Kiraia na sio ya Kipolisi:** Badala ya kutekeleza majukumu yake kama Askari, Wajibu wa Afisa Misitu Wilaya katika USMJ ni:-
 - ❖ Kutoa Ushauri wa kitaalamu kwa Serikali ya Kijiji na Kamati ya Maliasili
 - ❖ Ni daraja la kuunganisha Kijiji na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kuhusu misitu
 - ❖ Msuluhishi na mpatanishi baina ya jamii au kati ya Kijiji na Kijiji kuhusu maswala ya misitu
 - ❖ Mratibu, kati ya Kijiji na wadau wengine wa usimamizi wa msitu wa Kijiji
 - ❖ Mwangalizi – akitambua ni wakati gani aingilie jambo gani nani wakati gani awaache wanajamii watekeleze majukumu yao na wanufaike na rasilimali zao wenyewe

FAHAMU MISINGI YA KISHERIA KATIKA KUANZISHA NA KUTEKELEZA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA JAMII (USMJ)

Msingi wa Serikali za Vijiji kutekeleza USMJ, kwa kuanzisha Misitu ya Hifadhi za Vijiji, Misitu ya jamii au Vikundi au Hata Misitu ya Watu binafsi, unapatikana katika sheria zifuatazo:

- i) **Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999** – imeweka msingi wa Halmashauri ya kijiji kusimamia ardhi iliyo ndani ya mipaka ya kijiji
- ii) **Sheria ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya mwaka 2007** – Imeweka utaratibu wa Kijiji kupanga matumizi ya ardhi yake, kwa kadiri wanakijiji wanavyoona inafaa, ikiwezekana kutenga eneo la Misitu wa Hifadhi wa Kijiji
- iii) **Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998, Tamko namba 5 na 6** – imeweka utaratibu wa kurasimisha Misitu iliyo katika ardhi ya kijiji
- iv) **Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002, vifungu namba 32 hadi 41** – imeweka utaratibu wa kisheria wa kuanzisha Misitu wa Hifadhi wa Kijiji, Misitu wa Hifadhi wa Jamii au Kikundi na Misitu wa Hifadhi wa Mtu binafsi, katika ardhi ya kijiji
- v) **Kanuni za Misitu 2004** - zimeweka mwongozo wa kutekeleza utaratibu wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii (USMJ)
- vi) **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) 1982** – Imeweka utaratibu wa Kiutawala na Kiutendaji katika kusimamia rasilimali za kijiji

Kupanga bei ya Mazao ya Misitu: Kifungu namba 78 (3), cha Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002, kimetoa mamlaka kwa Serikali za Vijiji kupanga bei na kuuza mazao ya misitu ya Hifadhi za Vijiji kuendana na mazingira yao, bila kuingiliwa na mamlaka nyingine.

Wananchi Kumiliki Asilimia 100 ya mapato yanayotokana na mauzo ya mazao ya msitu wa Hifadhi wa Kijiji: Kijini kinaweza kutenga kiasi fulani cha mapato yake kwa ajili ya kulipia huduma za kitaalamu kutoka kwa maafisa wa serikali au wadau wengine. Kiasi hicho hupangwa na Kijiji chenyewe na sio mamlaka nyingine yoyote. Hata hivyo ni lazima Kijiji kilipe kodi kwa mujibu wa Sheria za nchi.

Kutoza na kumiliki mapato ya faini katika msitu wa hifadhi wa Kijiji: Mapato yote ya faini zinazotokana na wahalifu wanaokamatwa wakiharibu msitu wa Kijiji wanatozwa faini ambayo inakuwa mapato ya Kijiji kwa asilimia 100. Muhimu kwamba, faini hiyo iwe ni kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Usimamizi wa Msitu wa Kijiji zilizoidhinishwa.

Msamaha kuhusu Miti ya Iliyohifadhiwa: Kifungu namba 65(3) cha Sheria ya Misitu namba 14, ya mwaka 2002, kimetoa haki kwa Kijiji kumiliki na kusimamia miti yote iliyo katika Misitu wa Hifadhi wa Kijiji, ikiwa ni pamoja na Miti yenye hadhi maalumu, kiuchumi na kiikolojia, au iliyo katika hatari ya kutoweka.

Kutaifisha na Kuuza Mazao ya Msitu au Vifaa vilivyokutwa kwenye Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kinyume cha Sheria. Mamlaka haya yamewekwa kupitia kifungu namba 97 (1)(b)), ambapo Halmashauri ya Kijiji inaweza kutaifisha mazao yote yaliyokamatwa kwenye Msitu wa Hifadhi wa kijiji yakiwa yamevunwa kinyume cha Sheria, pamoja na vifaa vyote vilivyohusika, na kuuza kwa kuzingatia taratibu za kisheria na mapato yanayopatikana kuwa ya Serikali ya Kijiji kwa asilimia 100.

HATUA ZA KUENZISHA UVUNAJI ENDELEU KATIKA MSITU WA KIJJI

HATUA YA KWANZA

Kufanya tathmini ya rasilimali za misitu na kugawa kanda za matumizi mbalimbali




HATUA YA PILI

Kukubaliana kutenga maeneo ya msitu wa hifadhi wa kijiji kwa kutumia dhana ya usimamizi shirikishi wa misitu



HATUA YA TATU

Kuandaa na kupitisha mpango wa usimamizi wa msitu na sheria ndogo za kusimamia msitu wa hifadhi wa kijiji



HATUA YA NNE

Kuandaa mpango wa uvunaji endelevu wa mazao ya misitu katika eneo la msitu wa kijiji lililotengwa kwa ajili ya uvunaji






HATUA YA TANO

Kusimamia shughuli za uvunaji endelevu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali



KIJIJI KITAPATA NINI KUTOKANA NA UVUNAJI WA MISITU ILIYO NDANI YA MIPAKA YA KIJIJI?

Faida za kutenga maeneo kuwa misitu wa kijiji



Uvunaji kwenye eneo lililotengwa:

Kijiji kina haki ya kupata asilimia mia moja (100%) ya mapato yote yanayotokana na uvunaji endelevu unaofanyika katika eneo hili la msitu. Kibali hutolewa na Halmashauri ya Kijiji husika na uvunaji husimamiwa na kamati ya maliasili ya kijiji husika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Uvunaji kwenye eneo lisilotengwa:

Mapato yote yanayotokana na uvunaji unaofanyika kwenye msitu huu ni mali ya Serikali kuu au Halmashauri ya Wilaya kwa asilimia mia moja (100%) na kibali cha uvunaji hutolewa na kamati ya uvunaji ya wilaya kupitia kwa Halmashauri ya kijiji husika.

Ni vizuri kijiji kikatenga na kusimamia eneo lote la misitu iliyo ndani ya mipaka ya kijiji ili iweze kupata asilimia mia moja ya mapato yanayotokana na misitu hiyo kwa ajili ya shughuli za mandeleo ya kijiji na uhifadhi wa misitu

ZINGATIA MISINGI YA UTAWALA BORA KATIKA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA KIJJI CHAKO

1. Ushirikishwaji

- ❖ Andaa na Idhinisha bajeti na mpango kazi wa mwaka wa halmashauri na kamati ya maliasili kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji Miezi mitatu kabla mwaka mpya wa fedha haujaanza.
- ❖ Fanya vikao vya halmashauri na kamati ya maliasili kila mwanzo wa mwezi na Mkutano mkuu wa Kijiji wenye akidi kamili kila robo mwaka.
- ❖ Weka utaratibu wa kuhakikisha mikutano ya vitongoji yenye akidi kamili inafanyika mara kwa mara au kila mwezi.

2. Uwazi

- ❖ Tangeneza na simika mbao za matangazo kwenye Ofisi ya Kijiji, Kila kitongoji, na kwenye mikusanyiko ya watu wengi.
- ❖ Weka nakala ya bajeti ya Kijiji kwenye mbao za matangazo mwezi mmoja kabla mwaka mpya wa fedha haujaanza.
- ❖ Andaa na weka kwenye Mbao za Matangazo, ratiba ya Mikutano Mkuu ya Kijiji na ya Vitongoji kabla mwaka mpya wa fedha haujaanza.
- ❖ Toa taarifa za fedha na za utekelezaji wa kazi zikiwa sahihi, kamili na kwa wakati kwenye mkutano mkuu wa Kijiji kila robo mwaka na kwenye mbao za matangazo mara kwa mara, au angalau kila mwezi.
- ❖ Weka kwenye mbao za matangazo mchakato wote wa kuwapata wazabuni na watoa huduma wengine katika kutekeleza miradi ya Kijiji, na wanunuzi wa mazao ya Msitu wa Hifadhi wa Kijiji.

3. Uwajibikaji

- ❖ Hakikisha Hesabu za Fedha za Halmashauri na Kamati ya Maliasili zinakaguliwa kila mwaka kufikia mwezi Septemba.
- ❖ Rekebisha dosari zote zinazoibuliwa na wakaguzi na toa taarifa kwenye mkutano mkuu wa Kijiji kufikia mwezi Oktoba.
- ❖ Weka waangalizi au wadhhibi ndani ya kijiji kwa ajili ya kuthibitisha utekelezaji wa shughuli za Kijiji kila mwezi.
- ❖ Chukua hatua za kinidhamu dhidi ya viongozi waliokosa maadili, ikiwa ni Pamoja na kuwatoza faini na kuwaonya.

4. Utawala wa Sheria

- ❖ Weka utaratibu Madhubuti wa kusoma Sheria Ndogo za Kijiji katika kila kikao na mkutano wa Kijiji unapofanyika.
- ❖ Rejea na nukuu kipengele cha sheria kinachohusika kwa kila maamuzi yanayofanyika kijijini.
- ❖ Fanya doria mara kwa mara, anagalau mara mbili kila mwezi kwa ajili ya kulinda msitu wa Hifadhi wa Kijiji.
- ❖ Epuka kuidhinisha uvunaji katika maeneo ambayo hayajahifadhiwa kisheria kwani kifungu namba 46(4)(a) cha Sheria ya. Misitu no. 14 ya 2002 kimekataza uvunaji kufanyika kinyume na mpango wa usimamizi wa msitu husika.

5. Uadilifu

- ❖ Hakikisha shughuli zote za Kijiji zinazofanyika zinakuwa na Ufafanuzi wenye vithibitisho kamili na halali mfano stakabadhi za kukiri mapokezi, hati za malipo, risiti za manunuzi na mihtasari ya vikao.
- ❖ Kamwe usitumie fedha za Kijiji kabla hazijapelekwa benki.
- ❖ Kataa na epuka maswala ya rushwa, udangajifu, wizi na ubadhiriifu wa fedha na rasilimali nyingine za Kijiji.
- ❖ Tangaza kwenye mkutano na mbao za matangazo matukio yote ya uhalifu na hatua za kisheria zilizochukuliwa, hata kama matukio hayo yanamhusu kiongozi wa Kijiji au mkazi wa kijiji.
- ❖ Weka sanduku la maoni na mfumo huru ulio wazi wa kuchambua na kufanyia kazi maoni yanayotolewa.

6. Ufanisi na Tija

- ❖ Epuka kurudia rudia kazi hiyo hiyo kwa lengo la kulipwa mara mbili au kutengeneza mazingira ya kuchelewesha kazi ili kuongeza malipo. Mfano kufanya safari mbili wakati safari moja tu ingetosha kufanya kazi zote mbili.
- ❖ Zingatia kutanguliza matumizi ya fedha na rasilimali kwa ajili ya shughuli zinazonufaisha wananchi walio wengi.

7. Usawa

- ❖ Hakikisha angalau theluthi moja ya wajumbe wa kamati ya maliasili ni wanawake.
- ❖ Toa uwiano sawa kwa wanawake na wanaume katika kufanya maamuzi.
- ❖ Himiza vijana na wanawake kushiriki kwenye uongozi wa Kijiji.
- ❖ Epuka kuwabagua wajane, wasiojiweza, wenye ulemavu katika matumizi ya rasilimali za kijiji.


8. Mwitikio

- ❖ Himiza kila mwananchi kushiriki shughuli za usimamizi wa msitu wa Kijiji ikiwa ni Pamoja na kutoa taarifa za uhalifu na uharibifu wa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji.
- ❖ Kila mwananchi kushiriki mikutano, kuhoji, kuchangia mawazo, na kutekeleza miradi ya maendeleo ya kijiji.

9. Maridhiano

- ❖ Hakikisha hata kundi la walio wachache wanapata nafasi ya kusikilizwa katika kufanya maamuzi juu ya rasilimali za Kijiji.
- ❖ Epuka na tatua migogoro kwa njia ya mazungumzo na masikilizano.

WANAWAKE NA WANAUME WAPATIWE FURSA SAWA KATIKA KUFANYA MAAMUZI NA KUSIMAMIA RASILIMALI ZA KIJJI



Kifungu cha 33 (2) (b) cha Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002, kimeelekeza kamati ya maliasili iundwe kwa kuzingatia uwiano wa jinsia. Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii umeelekeza angalau theluthi moja ya wajumbe wa Kamati ya Maliasili wawe wanawake.

- **Wanawake na vijana ni nguzo muhimu katika utawala na uongozi wa kijiji. Wanapaswa kupewa nafasi muhimu za uongozi kama Mwenyekiti, Katibu au Mwekahazina wa Kamati ya Maliasili na kamati nyingine za Halmashauri ya Kijiji.**
- **Wanawake na vijana wanapaswa kupewa nafasi ya kutosha kufanya shughuli za usimamizi wa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji na biashara endelevu ya mazao ya Misitu.**

UTAWALA BORA KATIKA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA KIJJI!

Wajibu wako mwananchi ni nini?

1. Hakikisha Umeshiriki Mkutano Mkuu wa Kijiji kuidhinisha Bajeti na Mpango Kazi wa Mwaka wa kijiji chako na Kamati ya Maliasili, ndani ya Kipindi cha Miezi Mitatu kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa fedha,
2. Tembelea mbao za matangazo mara kwa mara, kila wiki na kila mwezi, kupata taarifa za maendeleo ya kijiji chako,
3. Hakikisha unafuatilia kwenye ofisi ya serikali ya kijiji na kupata ratiba au kalenda ya Mikutano Mikuu ya kijiji ya kila robo mwaka na ya mikutano ya kitongoji chako,
4. Shiriki Mkutano mkuu wa Kijiji kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya kufanya maamuzi kuhusu usimamizi wa rasilimali za kijiji chako,
5. Shiriki mikutano ya kitongoji chako ili kupata taarifa za mara kwa mara za maendeleo ya kijiji chako, kuibua hoja unazotoka zifanyiwe kazi kwa haraka na mapendekezo ya bajeti na mpango kazi wa kijiji chako,
6. Toa taarifa za uharibifu wa Msitu kwa kamati ya maliasili ya kijiji chako mapema kila unapozipata,
7. Tekeleza Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji na Mpango wa Usimamizi wa Msitu wa Kijiji na Sheria Ndogo zilizoandaliwa na Serikali ya Kijiji. Epuka kutumia ardhi ya kijiji kinyume na Maelekezo ya Mpango wa Matumizi bora ya ardhi au kufanya vitendo vya kukiuka Sheria Ndogo za Kijiji chako, ulizoziandaa mwenyewe,
8. Hoji ili kupata UFAFANUZI, UTHIBITISHO na UHALALISHO wa mwenendo wa Usimamizi wa Msitu, Fedha na Rasilimali nyingine za kijiji,
9. Kuhimiza UKAGUZI wa hesabu za fedha na rasilimali nyingine za kijiji kufanyika kufikia mwezi Septemba kila mwaka na kudai TAARIFA YA UKAGUZI na ya UTEKELEZAJI WA MAONI YA MKAGUZI iwasilishwe kwenye mkutano Mkuu wa kijiji kufikia mwezi Oktoba kila mwaka,
10. Tumia SANDUKU LA MAONI kuwasilisha kero au hoja ambazo hukuweza kuzifikisha kupitia mkutano mkuu wa kijiji,
11. Omba Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wilaya kufanya UKAGUZI MAALUM wa taarifa za Kijiji endapo mkutano mkuu wakijiji haukuridhishwanataarifazilizowasilishwa,
12. Toa taarifa kwa MAMLAKA ZA JUU, mfano Ofisi ya KATA, TARAFU au kwa MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA endapo kuna jambo ambapo viongozi wa kijiji wametenda kinyume na utaratibu na halikupata ufumbuzi ngazi ya kijiji.



JE! SERIKALI YA KIJJI CHAKO INATEKELEZA AINA GANI YA USHIRIKISHWAJI KATIKA KUSIMAMIA RASILIMALI ZA KIJJI?

Ushirikishwaji wa kujifanya, wa kinafiki, wa hila au wa kilaghai:

- ❖ Vikao au Mikutano ya Kijiji ya inaitishwa wakati maamuzi kuhusu jambo linalokusudiwa yamekwishafanyika.
- ❖ Wananchi hawapati nafasi ya kushawishi maamuzi mbadala bali wanaridhia kila kitu kilichowasilishwa na viongozi.
- ❖ Ushirikishwaji unafanyika kutimiza matakwa ya sheria tu ili kupata uhalali wa jambo lililokwisha amuliwa.
- ❖ Kuna wakati tunafanya mkutano, lakini ajenda ya jambo linalofichwa halitajwi, bali linaingizwa kwenye muhtasari ili kupata ushahidi wa kuomba idhini ya jambo hilo kutoka mamlaka za juu za serikali.
- ❖ Mikutano inafanyika kufanya maamuzi katika mazingira ambayo inajulikana wazi wananchi hawajaelimishwa vya kutosha hivyo wakafanya maamuzi ya jambo wasilolielewa barabara.
- ❖ Wananchi au wajumbe wenye uelewa mkubwa katika jamii wananyimwa fursa ya kushiriki vikao vya kufanya maamuzi au wananyimwa taarifa za kuwawezesha kufanya uchambuzi wa kina na kuhimiza maamuzi mbadala.

Ushirikishwaji uliosinyaa au Ushirikishwaji wa Taarifa au wa Matangazo.

- ❖ Vikao na Mikutano hufanyika kwa ajili ya kutoa taarifa, amri, maelekezo, makatazo au maagizo kwa wajumbe au wananchi.
- ❖ Hapatolewi nafasi ya kuwasikiliza walengwa, kuajadiliana nao kuhusu fursa na changamoto zilizopo, na mbinu mbadala za kufanya jambo husika ili kuleta matokeo mazuri zaidi.

Ushirikishwaji wa kukusanya Maoni:

- ❖ Sifa kuu ya aina hii ya ushirikishwaji ni **kusikiliza wananchi wanasemaje!**
- ❖ Maoni ya wananchi yanakusanywa kupitia vikao, mikutano, sanduku la maoni, au madodoso ya utafiti, lakini sio lazima yafanye kazi; yaani hailazimiki yatumike kwa ajili ya kuandaa mipango na kufanya maamuzi.
- ❖ Halmashauri ya kijiji inatoa mrejesho wa maoni ya wananchi yaliyopelekwa kwa viongozi wa juu kupitia warsha, barua, au mawasiliano ya ana kwa ana?
- ❖ Maoni yaliyotolewa na wananchi na ushauri

uliotolewa na wataalamu kupitia taarifa za ukaguzi au uchunguzi uliofanyika yanafanyiwa kazi na taarifa kutolewa kwa wananchi?

Ushirikishwaji wa zawadi:

- ❖ Wajumbe au wananchi kushiriki vikao na mikutano lakini ushiriki wao ni kwa sababu ya kupata zawadi au posho tu.
- ❖ Posho inaweza kutolewa kwa ajili ya kuhimiza uungwaji mkono, wa jambo lenye maslahi ya wachache.
- ❖ Mfano wafanya biashara wa mazao ya msitu, wanawezakulipaposhoyakikaochakuwaidhinisha, na mara nyingi wanaidhinishwa kuvuna maeneo ambayo hayajahifadhiwa, na hayana mipango ya uvunaji endelevu.

Ushirikishwaji wa Kutimiza Malengo:

- ❖ Kunakuwa na malengo fulani ambayo tayari yamekwishawekwa, lakini watendaji au wajumbe wa serikali ya kijiji au hata wadau wa maendeleo ya kijiji wakagundua kuwa, hakuna namna ya kufikia malengo hayo bila vikao au mikutano ya ushirikishwaji.

Ushirikishwaji wa kushirikishana na Kushauriana:

- ❖ Wananchi na wadau wengine wote kwa pamoja hushirikiana na viongozi wao na wataalamu, kutambua na kuchambua tatizo na fursa kwa pamoja, kuweka vipaumbele, kuandaa mpango kazi na kufanya maamuzi na kuyatekeleza.
- ❖ Ushirikishwaji wa namna hii huzalisha ubia baina ya kamati na halmashauri ya kijiji na wadau mbalimbali, katika kutekeleza mipango ya maendeleo.
- ❖ Ushirikishwaji wa namna hii hupelekea kutambua wadau wenye uzoefu na uwezo mkubwa wa kukabiliana na changamoto fulani kuliko wengine, na kwamba kwao changamoto hiyo ni fursa

Ushirikishwaji wa Kujenga uwezo:

- ❖ Kuweka maamuzi ya mwisho mikononi mwa wananchi. Kutekeleza kwa kadiri wananchi walivyoamua.
- ❖ Hii ni aina ya ushirikishwaji ambayo wananchi wenyewe huchukua hatu dhidi ya matatizo yao, bila kusubiri kuitwa au kuandaliwa mikakati na halmashauri ya kijiji au wataalamu.
- ❖ Serikali au wataalamu hutekeleza mipango ya wananchi au kuendeleza kazi zilizoanzishwa na wananchi wenyewe.

ZINGATIA MISINGI YA UTAWALA WA SHERIA KATIKA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA KIJJI CHAKO

SHERIA YA MISITU



- i) Hairuhusiwi serikali ya Kijiji kutekeleza shughuli za uvunaji wa mazao ya misitu nje ya msitu wa hifadhi wa kijiji
- ii) Hairuhusiwi kuidhinisha uvunaji wa mazao ya misitu kwenye maeneo ambayo hayajahifadhiwa katika ardhi ya Kijiji, kwani hayana mpango wa usimamizi wala uvunaji endelevu wa mazao ya misitu
- iii) Hairuhusiwi kuvuna miti ambayo ukubwa wake haujakidhi Kipenyo Kinachohitajika Kisheria.

*"Sheria ni Msumeno, hukata huku na huko"
Epuka vitendo vya rushwa na uvunaji haramu wa mazao ya msitu, Zingatia Sheria"*

Mambo ya kuzingatia katika Utawala wa Sheria Kijijini

- Kila mjumbe awe na nakala yake ya Sheria Ndogo za Kijiji. Toa nakala kwa wenyeviti wa vitongoji, wajumbe wa kamati na vijiji jirani
- Kabidhi nakala za Sheria Ndogo kwa wawasimamizi wa Sheria kama vile ofis ya kata, tarafa, kituo cha polisi, mahakama ya mwanzo.
- Kwa kila kikao na kila mkutano tujikumbushe vipengele muhimu vya sharia ndogo
- Kufanya marekebisha ya Sheria Ndogo kuendana na Mahitaji

Utekelezaji na Uzingatiaji wa Sheria

- Vibali halali vitolewe kuruhusu mambo yote yanayopaswa kufanyika kwa kibali
- Kila mhalifu anayekamatwa na kuadhibiwa asaini Hati ya kukiri kosa na adhabu

Katika kutoa adhabu kwa Mujibu wa Sheria, Serikali ya Kijiji inaweza

- Kutoa onyo au Karipio kwa mkosaji
- Kumtaka mkosaji ajieleze na kuomba radhi
- Kutoza faini kwa mujibu wa Sheria Ndogo
- Kumfukuza mkosaji kwenye nafasi ya uongozi



Katika Kusimamizi Msitu wa Hifadhi wa Kijiji, Serikali ya Kijiji lazima iandae Sheria Ndogo, kwa kuzingatia Madaraka iliyopewa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Malaka za Wilaya) ya 1982, katika vifungu vya 163 hadi 167

Mchakato wa kutunga sheria ndogo, na kuzisimamia uwe wa wazi, shirikishi na unaozingatia misingi ya haki za wananchi wote.

Katika kusimamia Sheria Serikali ya Kijiji inaweza

- i) Kufungua Kesi Polisi na Mahakamani - endapo kosa lililotendeka haliwezi kuamuliwa kwa kutumia Sheria ndogo au Mkosaji amegoma kutimiza adhabu aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Usimamizi wa Msitu wa Kijiji
- ii) Kuwa na Kitabu cha Orodha ya Makosa, ili kutunza kumbukumbu za uhalifu na uharibifu wa Rasilimali za Kijiji
- iii) Kuweka Wazi Taarifa za Uhalifu na Adhabu hata kama zinawahusu viongozi ili kukomesha uhalifu
- iv) Kuitisha Uthamini wa Mali au Rasilimali iliyoharibika au hasara iliyosababishwa na uhalifu
- v) Kuitisha Uchunguzi Maalum au Ukaguzi wa Nje, endapo jambo husika halina Ushahidi wa kutosha. Mara nyingi ukaguzi unafanyika kwa maswala yanayohusiana na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora au ubadhirifu wa fedha za kijiji



Muhimu kukumbuka:


- 1) Kila faini inayotozwa lazima iwe kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Kijiji. Hakikisha unanukuu kifungu husika cha Sheria kwenye Hati ya kukiri kosa, ambayo mkosaji atasaini
- 2) Fidia lazima iambatane na tathmini ya kitaalamu. Hakikisha unawasiliana na wataalamu husika ili kupata uthamini halisi wa hasara iliyosababishwa na mkosaji.
- 3) Kila tendo la usimamizi wa Sheria lazima liwe na uthibitisho halali uliowekwa kimaandishi

JE! MSITU WA HIFADHI WA KIJIKI CHAKO UMETANGAZWA KWENYE GAZETI LA SERIKALI?

Kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14, 2002 kifungu cha 32 (1); Serikali ya Kijiji itakuwa na uhalali wa kumiliki Msitu wa Hifadhi katika Ardhi ya Kijiji endapo msitu huo:

- Utakuwa umetangazwa na kusajiliwa kwenye daftari la halmashauri husika; na/au
- Utakuwa umetangazwa kwenye Gazeti la Serikali (GN);

Kwa kuzingatia Kifungu namba 35 (1) cha Sheria ya Misitu Na. 14 ya 2002, Serikali ya Kijiji ikishasimamia Msitu wa Hifadhi wa Kijiji uliotangazwa na kusajiliwa kwenye daftari la Halmashauri ya Wilaya husika, kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (3); inaweza kupeleka Maombi ya Kutangaza Msitu huo kwenye Gazeti la Serikali. Maombi yatapelekwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya.



Hatua za Kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kwenye Gazeti la Serikali

Hatua ya 1:

Kijiji kitaanda maombi yenye viambatanisho vifuatavyo, kumwomba Mkurugenzi wa idara ya Misitu na Nyuki kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Kijiji kwenye gazeti la Serikali.

- Muhtasari wa mkutano mkuu wa kijiji ulioazimia kuanzishwa kwa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji;
- Majina ya Wajumbe wa Kamati ya Maliasili au chombo kingine kilichowekwa kwa mujibu wa vifungu namba 33 (1) (d), (2) na 34 (3) vya Sheria Ya Misitu Na. 14, 2002;
- Ramani Rasmi au ushahidi wa kimaandishi unaonesha mipaka ya Ardhi ya Kijiji; Msitu wa Hifadhi wa Kijiji na Vijiji Jirani vinavyopakana nao;
- Nakala ya mpango wa Usimamizi wa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji;
- Nakala rasmi ya Sheria ndogo ya Usimamizi wa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji;
- Maelezo mafupi ya sababu ya kijiji kuomba kutangaza msitu wake kwenye gazeti la Serikali na madhumuni ya kuanzisha Msitu huo kuwa Hifadhi ya Kijiji;
- Maelezo mafupi kuhusu utaratibu wa usimamizi wa fedha zitokanazo na Msitu wa Hifadhi wa Kijiji;
- Maelezo mafupi ya watumishi walioajiriwa na halmashauri ya kijiji ili kusimamia msitu wa hifadhi wa kijiji (Kama wapo).

Hatua ya 2:

Serikali ya Kijiji itapeleka maombi kwa Mkurugenzi wa halmashauri ya husika, ambaye atayahakiki na kutoa taarifa ya matokeo ya uhakiki huo ndani ya kipindi cha siku 60 tangu tarehe ya kupokea maombi hayo kutoka kijijini.

Hatua ya 3:

Endapo Maombi ya Kijiji yatakuwa hayana dosari yoyote Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika atayawasilisha kwa Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki kwa niaba ya Serikali ya kijiji.

Hatua ya 4:

Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, ataamua ama kukubali maombi ya kijiji bila masharti au kwa masharti na atatoa sababu za masharti hayo, na kama atakataa maombi pia atatoa sababu.

Hatua ya 5:

- Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki
- ataitaarifu halmashauri ya kijiji husika matokeo ya maombi yao;
 - kama maombi yamekidhi vigezo vyote atautangaza Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kwenye **GAZETI LA SERIKALI (GN)**.

Faida za Kutanga Msitu wa Hifadhi wa Kijiji Kwenye Gazeti la Serikali

- Kurasimisha zaidi Msitu wa Hifadhi wa Kijiji na kuufanya ujulikane zaidi kitaifa na kimataifa
- Kuupa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji hadhi ya juu na kuufanya uheshimike zaidi kisheria

URAGHIBISHI

USHAWISHI SERA, MIPANGO NA MAAMUZI

1.0 URAGHIBISHI NI NINI?

Uraghibishi ni mkakati wa kushawishi watu wanaofanya maamuzi yanayogusa maslahi ya wengi katika Serikali, Taasisi au Asasi mbalimbali ili ser, mipango au maamuzi yanayofanyika yawe na manufaa kwa umma.

2.0 MAMBO MUHIMU KATIKA URAGHIBISHI

→ Uraghibishi (ushawishi hauna mwisho. Kila wakati kuna sera au mipango inayohitaji kuboreshwa ili kutatua matatizo mbalimbali ya jamii

→ Uraghibishi hujumuisha vitendo vya kushawishi vilivyopangwa kwa utaratibu maalum

→ Uraghibishi hulenga kujenga makubaliano katika kundi la watu au asasi mbalimbali ili kushawishi

→ Uraghibishi hulenga kuanzisha, kubadilisha au kutekeleza sera

3.0 SERA YA NCHI NI NINI?

Sera ya nchi ni mwongozo rasmi wa Serikali wenye lengo la kushughulikia masuala maalumu ya jamii. Uraghibishi hulenga kushawishi ili sera nzuri za misitu zitekelezwe kikamilifu. Wadau huweza kufanya ushawishi ili mipango shirikishi ya kuhifahi misitu itekelezwe

4.0 NYENZO ZA URAGHIBISHI

- ✍ Elimu kwa Umma
- ✍ Kujenga mitandao na mahusiano
- ✍ Majadiliano na mikutano kuhusu suala husika
- ✍ Kuhamasisha Wadau
- ✍ Ili kutumia vizuri nyenzo za uraghibishi, ni muhimu kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu SERA na masuala muhimu ya kisiasa

5.0 MPANGO WA URAGHIBISHI

Zifuatazo ni hatua/maswali muhimu ya kujiuliza katika mkakati wa Uraghibishi (ushawishi)

- Tatizo au suala linalohitaji ushawishi ni lipi?
- Kwa njia ipi utalielewa kwa undani tatizo au suala husika
- Nini malengo ya mkakati wa Uraghibishi?
- Utashirikiana na nani ili kushawishi?
- Ni njia zipi zitatumika ili kufanikisha mkakati wa kushawishi?
- Utekelezaji wa mpango wa uraghibishi
- Tathmini ya mafanikio/matatizo ya mkakati ili Kuboresha.



Kamati ya Maliasili ya kijiji wakijadiliana na Maafisa Misitu kuhusu mipango shirikishi ya kuhifadhi misitu

URAGHIBISHI

USHAWISHI KUHUSU SERA, MIPANGO NA MAAMUZI HATUA MUHIMU KATIKA MPANGO WA URAGHIBISHI

1. Kutambua tatizo au swala linalohitaji ushawishi (Hakuna matumizi endelevu ya misitu)



2. Njia ya kuelewa kwa undani tatizo au swala husika (Sera ya misitu hitekelezi ipasavyo)



7. Tathmini ya mafanikio ya mkakati wa uraghibishi (Je lengo limetekelezwa? Tatizo bado lipo? Nini kifanyike?)

3. Lengo na ujumbe wa mkakati wa uraghibishi



7. Utekelezaji wa mkakati wa uraghibishi (Majadiliano kati ya wanajamii wanaoishi pembezoni mwa msitu na maafisa msitu)



5. Njia za kufanikisha mkakati wa uraghibishi

NYENZO/ NJIA ZA URAGHIBISHI

- Elimu kwa umma
- Kujenga mitandao na mahusiano
- Majadiliano na mikutano kuhusu swala husika
- Kuhamasisha wadau



4. Utashirikiana na nani ili kushawishi

URAGHIBISHI

USHAWISHI KUHUSU SERA, MIPANGO NA MAAMUZI



1. KUANDIKA BARUA

- Andika barua kwa kiongozi anayehusika katika eneo lako
- Eleza shida au kero kwa ufasaha
- Acha nakala kwa kumbukumbu zako hakikisha ina tarehe
- Piga simu kufuatilia majibu

2. KUPIGA SIMU

- Uwe na dondoo mbele yako ili uongee kwa kifupi
- Eleza vizuri tatizo lililofanya upige simu na athari zake
- Eleza unataka kiongozi afanye nini kuhusu tatizo hilo
- Uliza lini uamuzi au hatua zitachukuliwa



TUNAFUTILIA UTEKELEZAJI WA SERA KAMA TULIYOONGEA KWA SIMU JUZI



2. MKUTANO NA VIONGOZI

- Panga muda na mtu sahihi wa kukutana naye
- Mjulishe kitakachozungumziwa
- Eleza tatizo kwa ufasaha
- Mwambie kiongozi unataka ofisi ya ifanye nini
- Omba jibu kwa tarehe maalum

Rushwa ni adui wa misitu



RUSHWA NI ADUI KATIKA USIMAMIZI ENDELEU WA MISITU YETU!

Asilimia 82 ya wadau waliohojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mwaka 2013, walikiri uwepo wa Rushwa katika Uvunaji na Usafirishaji wa Mazao ya Misitu Tanzania. Hii ni pamoja na

- Kuvuna au usafirisha mazao ya misitu bila kibali halali, au kughushi nyaraka za uvunaji na usafirishaji.
- Kuvuna na Kusafirisha miti isiyoruhusiwa, ambayo haijakomaa, au haijafikia kipenyo cha miti inayotakiwa kuvunwa kisheria
- Kuzidisha kiasi kilichoidhinishwa kwa mujibu wa mpango wa uvunaji, leseni au hati ya kusafirishia
- Kuidhinisha Uvunaji katika maeneo ambayo hayana Mpango wa Usimamizi wa Msitu

Epuka rushwa katika uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu! Linda misitu iliyo katika ardhi ya kijiji chako

Mpango wa Uvunaji Endelevu kwa misitu iliyo ndani ya Kijiji ujadiliwe kwenye mkutano mkuu wa Kijiji. Epuka kuidhinisha uvunaji wa misitu bila kuzingatia mpango wa uvunaji endelevu

Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji WASIPOKEE POSHO YA KIKAO kutoka kwa Wafanyabiashara wanaotaka kuidhinishwa kuvuna kijijini. Posho inaweza kuwashawishi kuidhinisha uvunaji kwenye maeneo ambayo hayaruhusiwi

Nakala ya mpango wa uvunaji, orodha ya Wateja waliomba, na walioidhinishwa kuvuna, aina na kiasi cha miti walichoidhinishwa lazima ibandikwe kwenye mbao za matangazo Kijijini.

Mazao ya misitu yaliyovunwa yahakikiwe na zaidi ya mtu mmoja, kabla hayajatolewa msitu. Visiki na Magogo vigongwe alama ya nyudo baada ya kuhakikiwa na kabla havijatolewa msituni.

Kikosi cha doria cha Kijiji kisiruhusiwe kutoza faini au kuchukua fedha kutoka kwa watuhumiwa wanaokamatwa, bali zitozwe ofisini kwa mujibu wa Sheria Ndogo za usimamizi wa Msitu wa Kijiji

Hakikisha taarifa za mnada zimetangazwa ndani na nje ya Kijiji, Mnada unafanyika kwa njia ya wazi na taarifa ya mnada inawasilishwa kwenye mkutano mkuu wa Kijiji.

Wagombea wa nafasi za uongozi wasitoe ahadi za kugawa Msitu wa Hifadhi kwa wakulima au wafugaji ili kupata kura. Wenyeviti na Watendaji wa vijiji, madiwani, wabunge au viongozi wa vyama vya siasa hawana mamlaka ya kugawa ardhi ya Kijiji kwa mtu yeyote kisheria.

Katika uvunaji endelevu,

Hairuhusiwi kuvuna miti ambayo haipo kwenye mpango wa uvunaji au kuzidisha kiwango kilichopo kwenye mpango wa uvunaji au leseni

Miti hupimwa kabla ya kuvunwa, visiki vya miti iliyovunwa, magogo na/au mbao huhakikiwa na kugongwa alama ya nyundo kabla ya kutolewa msituni



Imeandaliwa na Mradi wa Haki Katika Misitu (Forest Justice in Tanzania (FJT) Project)
Kwa mawasiliano zaidi andika kwa;



Mkurugenzi Mtandaji, Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG),
S.L.P 23410 Dar es Salaam, Tanzania; Simu: +255 22 2669007;
Barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz; tovuti: <http://www.tfcg.org>



Mkurugenzi Mtandaji; Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa
Misitu Tanzania (MJUMITA);
S.L.P. 21522 Dar-es-Salaam – Tanzania; tovuti: www.mjumita.org
Barua pepe: mjumitaorg@mjumita.org